# Sefania

1 Neno la Mwenyezi Mungu lililomjia Sefania
mwana wa Kushi, mwana wa Gedalia, mwana wa
Amaria, mwana wa Hezekia, wakati wa utawala
wa Yosia mwana wa Amoni mfalme wa Yuda:

*Onyo la maangamizi yanayokuja*

2 Mwenyezi Mungu asema,
“Nitafagia kila kitu
kutoka uso wa dunia.
3 Nitafagilia mbali watu na wanyama;
nitafagilia mbali ndege wa angani
na samaki wa baharini.
Wafanyao maovu watapata tu kokoto,
nami nitamkatilia mbali mwanadamu atoke katika dunia,”
asema Mwenyezi Mungu.

*Dhidi ya Yuda*

4 “Nitaiadhibu Yuda
na wote wanaoishi Yerusalemu.
Kutoka mahali hapa nitakatilia mbali
kila mabaki ya Baali,
majina ya wapagani na makuhani
waabuduo sanamu:
5 wale ambao husujudu juu ya mapaa
kuabudu jeshi la vitu vya angani,
wale ambao husujudu na kuapa kwa Mwenyezi Mungu
na ambao pia huapa kwa Malkamu,
6 wale wanaoacha kumfuata Mwenyezi Mungu,

wala hawamtafuti Mwenyezi Mungu
wala kutaka shauri lake.
7 Nyamazeni mbele za Bwana Mungu Mwenyezi,
kwa maana siku ya Mwenyezi Mungu iko karibu.
Mwenyezi Mungu ameandaa dhabihu,
amewaweka wakfu wale aliowaalika.
8 Katika siku ya dhabihu ya Mwenyezi Mungu
nitawaadhibu wakuu
na wana wa mfalme
na wale wote wanaovaa
nguo za kigeni.
9 Katika siku hiyo nitaadhibu wote ambao
hukwepa kukanyaga kizingiti,
ambao hujaza hekalu la miungu yao
kwa dhuluma na udanganyifu."

10 Mwenyezi Mungu asema, "Katika siku hiyo
kilio kitapanda juu kutoka lango la Samaki,
maombolezo kutoka mtaa wa pili,
na mshindo mkubwa kutoka vilimani.
11 Ombolezeni, ninyi mnaoishi katika eneo la sokoni;
wafanyabiashara wenu wote wameangamizwa,
wote ambao wanafanya biashara ya fedha
wataangamizwa.
12 Wakati huo nitaupekua mji wa Yerusalemu kwa taa,
na kuwaadhibu wale ambao
wanakaa katika hali ya kuridhika,
ambao ni kama divai
iliyobaki kwenye machicha,

ambao hudhani, ‘Mwenyezi Mungu hatafanya lolote,
jema au baya.’
13 Utajiri wao utatekwa nyara,
nyumba zao zitabomolewa.
Watajenga nyumba,
lakini hawataishi ndani yake;
watapanda mizabibu
lakini hawatakunywa divai yake.

### *Siku kubwa ya Mwenyezi Mungu*

14 “Siku kubwa ya Mwenyezi Mungu iko karibu:
iko karibu na inakuja haraka.
Sikilizeni! Kilio katika siku ya Mwenyezi Mungu
kitakuwa chungu.
Shujaa atapiga ukelele wa vita huko.
15 Siku ile ni siku ya ghadhabu,
siku ya fadhaa na dhiki,
siku ya uharibifu na ukiwa,
siku ya giza na utusitusi,
siku ya mawingu na giza nene,
16 siku ya tarumbeta na kelele za vita
dhidi ya miji yenye ngome,
na dhidi ya minara mirefu.
17 Nitawaletea watu dhiki,
nao watatembea kama vipofu,
kwa sababu wametenda dhambi
dhidi ya Mwenyezi Mungu.
Damu yao itamwagwa kama vumbi
na matumbo yao kama kinyesi.
18 Fedha yao wala dhahabu yao
hazitaweza kuwaokoa
katika siku hiyo ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

Katika moto wa wivu wake
dunia yote itateketezwa,
kwa maana ghafula ataleta mwisho
wa wote wanaoishi duniani.”

# 2

*Hukumu dhidi ya mataifa*

*Dhidi ya Yuda*

1 Kusanyikeni pamoja, kusanyikeni pamoja,
enyi taifa lisilo na aibu,
2 kabla wakati ulioamriwa haujafika
na siku ile inayopeperusha kama makapi,
kabla hasira kali ya Mwenyezi Mungu haijaja juu yenu,
kabla siku ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu
haijaja juu yenu.
3 Mtafuteni Mwenyezi Mungu, enyi nyote wanyenyekevu wa nchi,
ninyi ambao hufanya lile analoamuru.
Tafuteni haki, tafuteni unyenyekevu;
labda mtahifadhiwa
siku ya hasira ya Mwenyezi Mungu.

*Dhidi ya Ufilisti*

4 Gaza utaachwa
na Ashkeloni utaachwa magofu.
Wakati wa adhuhuri Ashdodi utaachwa mtupu,
na Ekroni utang’olewa.
5 Ole wenu ninyi ambao mnaishi kando ya bahari,
enyi Wakerethi;
neno la Mwenyezi Mungu liko dhidi yenu,

ee Kanaani, nchi ya Wafilisti.
“Mimi nitawaangamiza,
na hakuna atakayebaki.”
6 Nchi iliyo karibu na bahari itakuwa malisho
yenye visima vya wachungaji,
na mazizi ya kondoo.
7 Itakuwa mali ya mabaki ya nyumba ya Yuda,
hapo watapata malisho.
Wakati wa jioni watajilaza chini
katika nyumba za Ashkeloni.
Mwenyezi Mungu, Mungu wao, atawatunza,
naye atawarudishia wafungwa wao.

### *Dhidi ya Moabu na Amoni*

8 “Nimeyasikia matukano ya Moabu
nazo dhihaka za Waamoni,
ambao waliwatukana watu wangu
na kutoa vitisho dhidi ya nchi yao.
9 Hakika, kama niishivyo,”
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
Mungu wa Israeli,
“hakika Moabu itakuwa kama Sodoma,
Waamoni kama Gomora:
mahali pa magugu na mashimo ya chumvi,
nchi ya ukiwa milele.
Mabaki ya watu wangu watawateka nyara;
mabaki ya taifa langu watarithi nchi yao.”

10 Hiki ndicho watarudishiwa kwa ajili ya kiburi chao,
kwa kutukana na kudhihaki
watu wa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni.

11 Mwenyezi Mungu atakuwa wa kuhofisha kwao
atakapoangamiza miungu yote ya nchi.
Mataifa katika kila pwani yatamwabudu,
kila moja katika nchi yake.

### *Dhidi ya Kushi*

12 “Ninyi pia, ee Wakushi,
mtauawa kwa upanga wangu.”

### *Dhidi ya Ashuru*

13 Mungu atanyoosha mkono wake dhidi ya kaskazini
na kuangamiza Waashuru,
akiiacha Ninawi ukiwa
na pakame kama jangwa.
14 Makundi ya kondoo na ng’ombe yatajilaza pale,
viumbe vya kila aina.
Bundi wa jangwani na bundi waliao kwa sauti nyembamba
wataishi juu ya nguzo zake.
Mwangwi wa kuita kwao utapita madirishani,
kifusi kitakuwa milangoni,
boriti za mwerezi zitaachwa wazi.
15 Huu ndio mji uliotukuka na kuishi kwa furaha
wakijisikia salama.
Ulisema moyoni mwako,
“Mimi ndimi, na wala hapana mwingine ila mimi.”
Jinsi gani umekuwa gofu,
mahali pa kulala wanyama pori!
Wote wanaopita kando yake wanauzomea
na kutikisa mkono kwa dharau.

# 3

## *Maisha ya baadaye ya Yerusalemu*

### *Hatima ya Yerusalemu*

1 Ole mji wa wadhalimu,
waasi na waliotiwa unajisi!
2 Hautii mtu yeyote,
haukubali maonyo.
Haumtumaini Mwenyezi Mungu,
haukaribii karibu na Mungu wake.
3 Maafisa wake ni simba wanaonguruma,
watawala wake ni mbwa-mwitu wa jioni,
ambao hawabakizi chochote
kwa ajili ya asubuhi.
4 Manabii wake ni wenye kiburi,
ni wadanganyifu.
Makuhani wake hunajisi patakatifu
na kuihalifu sheria.
5 Mwenyezi Mungu aliye ndani yake ni mwenye
haki,
hafanyi kosa.
Asubuhi kwa asubuhi hutoa haki yake,
kila kukipambazuka huitimiza,
bali mtu dhalimu hana aibu.

### *Yerusalemu yakataa kutubu*

6 “Nimeyaangamiza mataifa,
ngome zao zimebomolewa.
Nimeziacha barabara ukiwa,
hakuna anayepita humo.
Miji yao imeharibiwa;
hakuna mmoja atakayeachwa:
hakuna hata mmoja.
7 Niliuambia huo mji,

‘Hakika utaniogopa na kukubali maonyo!’
Ndipo makao yake hayatafutiliwa mbali,
wala adhabu zangu zote hazitakuja juu yake.
Lakini walikuwa bado na shauku
kutenda kwa upotovu katika yote waliyofanya.”
8 Mwenyezi Mungu anasema,
“Kwa hiyo ningojee mimi,
siku nitakayosimama kuteka nyara.
Nimeamua kukusanya mataifa,
kukusanya falme
na kumimina ghadhabu yangu juu yao,
hasira yangu kali yote.
Dunia yote itateketezwa
kwa moto wa hasira yangu yenye wivu.

### *Mabaki ya Israeli kurejeshwa*

9 “Ndipo nitatakasa midomo ya mataifa,
kwamba wote waweze kuliitia jina la Mwenyezi Mungu
na kumtumikia kwa pamoja.
10 Kutoka ng’ambo ya mito ya Kushi
watu wangu wanaoniabudu,
watu wangu waliotawanyika,
wataniletea sadaka.
11 Siku hiyo hutaaibishwa
kwa ajili ya makosa yote uliyonitendea,
kwa sababu nitawaondoa kutoka mji huu
wale wote wanaoshangilia
katika kiburi chao.
Kamwe hutajivuna tena
katika kilima changu kitakatifu.
12 Lakini nitakuachia ndani yako
wapole na wanyenyekevu,

ambao wanatumaini jina la Mwenyezi Mungu.
13 Mabaki ya Israeli hayatafanya kosa;
hawatasema uongo,
wala udanganyifu hautakuwa
katika vinywa vyao.
Watakula na kulala
wala hakuna yeyote
atakayewaogopesha."

14 Imba, ee Binti Sayuni;
paza sauti, ee Israeli!
Furahi na kushangilia kwa moyo wako wote,
ee Binti Yerusalemu!
15 Mwenyezi Mungu amekuondolea adhabu yako,
amewarudisha nyuma adui zako.
Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Israeli, yu pamoja nawe;
kamwe hutaogopa tena madhara yoyote.
16 Katika siku hiyo watauambia Yerusalemu,
"Usiogope, ee Sayuni;
usiiache mikono yako ilegee.
17 Mwenyezi Mungu, Mungu wako, yu pamoja nawe,
yeye ni Shujaa mwenye nguvu anayeokoa.
Atakufurahia kwa furaha kubwa,
atakutuliza kwa pendo lake,
atakufurahia kwa kuimba."

18 "Huzuni katika sikukuu zilizoamriwa
nitaziondoa kwenu;
hizo ni mzigo na fedheha kwenu.
19 Wakati huo nitawaadhibu
wote waliokudhulumu;

nitaokoa vilema na kukusanya
wale waliotawanywa.
Nitawapa sifa na heshima
katika kila nchi ambayo waliaibishwa.
20 Wakati huo nitawakusanya;
wakati huo nitawaleta nyumbani.
Nitawapa sifa na heshima
miongoni mwa mataifa yote ya dunia
wakati nitakapowarudishia mateka yenu
mbele ya macho yenu hasa,”
asema Mwenyezi Mungu.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 13 Dec 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d